

Neno la Jumapili, 31. Agosti 2014

Wana ni urithi utokao kwa BWANA, watoto ni zawadi
kutoka kwake.

Zaburi 127,3

Ninyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu,
bali waleeni kwa nidhamu na mafundisho ya Bwana.

Waefeso 6,4

Behold, children are a heritage from the Lord.

Psalm 127:3 (ESV)

Fathers, do not provoke your children to anger,
but bring them up in the discipline
and instruction of the Lord.

Ephesians 6:4 (ESV)

Scriptures taken from Kiswahili Contemporary Version 
Copyright (c) 1984, 1989, 2006 by International Bible Society(R)
Used by permission. All rights reserved worldwide.

Neno la Ijumaa, 29. Agosti 2014

Usiwe kama farasi au nyumbu wasio na akili,
ambao ni lazima waongozwe kwa
lijamu na hatamu la sivyo hawatakaribia.

Zaburi 32,9

BWANA Mungu wenu ni mwenye neema na huruma.
Hatageuzia uso wake mbali nanyi
kama ninyi mkimrudia Yeye.

2 Mambo ya Nyakati 30,9

Be not like a horse or a mule, without understanding,
which must be curbed with bit and bridle,
or it will not stay near you.

Psalm 32:9 (ESV)

The Lord your God is gracious and merciful
and will not turn away his face from you,
if you return to him.

2 Chronicles 30:9 (ESV)

Neno Agosti 2014 The Word August 2014



Kiswahili Contemporary Version 2006
English Standard Version



Project Bible 2.0 www.bible2.net

Neno la Jumamosi, 2. Agosti 2014

Wakati alipokaribia lile tundu,
alimwita Danieli kwa sauti ya uchungu,
“Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je,
Mungu wako unayemtumikia daima,
ameweza kukuokoa na simba hawa?”

Danieli 6,20

BWANA akamjibu Mose,
“Je! Mkono wa BWANA ni mfupi sana?
Sasa utaona kama jambo nililolisema
halitatimizwa kwa ajili yako au la.”

Hesabu 11,23

King Darius declared to Daniel,
O Daniel, servant of the living God,
has your God, whom you serve continually,
been able to deliver you from the lions?

Daniel 6:20

And the Lord said to Moses,
Is the Lord's hand shortened?
Now you shall see whether my word
will come true for you or not.

Numbers 11:23 (ESV)

Neno la Jumatano, 27. Agosti 2014

Ndipo Mose akainua mkono wake
na kuupiga mwamba mara mbili kwa fimbo yake.
Maji yakabubujika, jumuiya na mifugo yao wakanywa.

Hesabu 20,11

na wote wakanywa kile kinywaji cha roho,
kwa maana walikunywa kutoka
katika ule mwamba wa roho uliofuatana nao,
ule mwamba ulikuwa Kristo.

1 Wakorinto 10,4

Moses lifted up his hand
and struck the rock with his staff twice,
and water came out abundantly,
and the congregation drank, and their livestock.

Numbers 20:11

The Israelites drank
from the spiritual Rock that followed them,
and the Rock was Christ.

1 Corinthians 10:4

Neno la Jumatatu, 25. Agosti 2014

Bwana aongea na Abram:

Mimi nitakufanya taifa kubwa na nitakubariki,
Nitalikuza jina lako, nawe utakuwa baraka.

Mwanzo 12,2

Nitamimina maji juu ya nchi yenye kiu
na vijito vya maji juu ya ardhi iliyokauka,
nitamimina Roho wangu juu ya watoto wako,
nayo baraka yangu juu ya wazao wako.

Isaya 44,3

The Lord said to Abram:

I will bless you and make your name great,
so that you will be a blessing.

Genesis 12:2 (ESV)

I will pour water on the thirsty land,
and streams on the dry ground;
I will pour my Spirit upon your offspring,
and my blessing on your descendants.

Isaiah 44:3 (ESV)

Neno la Jumatatu, 4. Agosti 2014

Mtu mwenye haki kweli kweli hupata uzima,
bali yeye afuatiliaye ubaya huendea kifo chake.

Mithali 11,19

Ingieni kwa kupitia mlango mwembamba,
kwa maana lango ni pana
na njia ni pana ielekeayo upotevuni,
nao ni wengi waingiao kwa kupitia lango hilo.

Mathayo 7,13

Whoever is steadfast in righteousness will live,
but he who pursues evil will die.

Proverbs 11:19 (ESV)

Enter by the narrow gate.
For the gate is wide and the way is easy
that leads to destruction,
and those who enter by it are many.

Matthew 7:13 (ESV)

Neno la Jumatano, 6. Agosti 2014

Mose akamjibu Farao,
"Nitakapokuwa nimetoka nje ya mji,
nitanyoosha mikono yangu juu kumwomba BWANA.
Ngurumo zitakoma na hapatakuwepo mvua ya mawe tena,
ili upate kujua kuwa, nchi ni mali ya BWANA."

Kutoka 9,29

Ee BWANA Mwenyezi, umeumba mbingu na nchi kwa
uwezo wako mkuu na kwa mkono ulionyoosha.

Hakuna jambo lililo gumu usiloliweza.

Yeremia 32,17

Moses said to Pharaoh,
As soon as I have gone out of the city,
I will stretch out my hands to the Lord.
The thunder will cease, and there will be no more hail,
so that you may know that the earth is the Lord's.

Exodus 9:29 (ESV)

Ah, Lord God!
It is you who have made the heavens and the earth
by your great power and by your outstretched arm!
Nothing is too hard for you.

Jeremiah 32:17 (ESV)

Neno la Jumamosi, 23. Agosti 2014

Waisraeli wote waume kwa
wake waliokuwa wanapenda wakaleta
mbele za BWANA kwa hiari yao wenyewe sadaka kwa ajili ya
kazi yote ya BWANA aliyokuwa
amewaagiza kuifanya kupitia kwa Mose.
Kutoka 35,29

Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu.
2 Wakorinto 9,7

All the men and women, the people of Israel,
whose heart moved them to bring anything for the work
that the Lord had commanded by Moses to be done
brought it as a freewill offering to the Lord.
Exodus 35:29 (ESV)

God loves a cheerful giver.
2 Corinthians 9:7 (ESV)

Neno la Alhamisi, 21. Agosti 2014

Atahukumu kati ya mataifa mengi
na ataamua migogoro ya mataifa
yenye nguvu na yaliyo mbali.
Watafua panga zao ziwe majembe
ya kulimia na mikuki yao kuwa miundu ya kukatia matawi.
Taifa halitachukua upanga dhidi ya taifa,
wala hawatajifunza vita tena.
Mika 4,3

Kwa Mungu mambo yote yanawezekana.
Mathayo 19,26

He shall judge between many peoples,
and shall decide for strong nations far away;
and they shall beat their swords into plowshares,
and their spears into pruning hooks;
nation shall not lift up sword against nation,
neither shall they learn war anymore.
Micah 4:3 (ESV)

With God all things are possible.
Matthew 19:26 (ESV)

Neno la Ijumaa, 8. Agosti 2014

Bartimayo akaanza kupaza sauti akisema,
"Yesu, Mwana wa Daudi, unihurumie!"
Marko 10,47

Ee BWANA, Wewe ni mwema na mwenye kusamehe,
umejaa upendo kwa wote wakuitao.
Zaburi 86,5

Bartimaeus, a blind beggar, began to cry out and say,
Jesus, Son of David, have mercy on me!
Mark 10:47 (ESV)

You, O Lord, are good and forgiving,
abounding in steadfast love to all who call upon you.
Psalms 86:5 (ESV)

Neno la Jumapili, 10. Agosti 2014

Fanyeni hukumu za haki,
onyesheni rehema na huruma ninyi kwa ninyi.
Zekaria 7,9

Huwapigania yatima na wajane,
humpenda mgeni akimpa chakula na mavazi.
Nanyi wapendeni wageni,
kwa kuwa ninyi wenyewe mlikuwa wageni huko Misri.
Kumbukumbu La Torati 10,18-19

Render true judgments,
show kindness and mercy to one another.
Zechariah 7:9 (ESV)

The Lord your God executes justice
for the fatherless and the widow,
and loves the sojourner, giving him food and clothing.
Love the sojourner, therefore,
for you were sojourners in the land of Egypt.
Deuteronomy 10:18-19 (ESV)

Neno la Jumanne, 19. Agosti 2014

BWANA awawezeshe kuongezeka,
ninyi na watoto wenu.
Zaburi 115,14

Peter akasema to the Jews:
Ninyi ndio wana wa manabii
na wa agano ambayo Mungu alifanya baba zenu,
akimwambia Abrahamu,
'Katika wewe, jamaa zote za duniani watabarikiwa.'
Matendo ya Mitume 3,25

May the Lord give you increase,
you and your children!
Psalm 115:14 (ESV)

Peter said to the Jews:
You are the sons of the prophets
and of the covenant that God made with your fathers,
saying to Abraham, "And in your offspring
shall all the families of the earth be blessed."
Acts 3:25 (ESV)

Neno la Jumapili, 17. Agosti 2014

Kila mmoja wenu asiangalie mambo yake mwenyewe tu,
bali pia ajishughulisha kwa faida ya wengine.
Wafilipi 2,4

Msidaiwe kitu na mtu ye yote,
isipokuwa kupendana,
kwa maana yeye ampendaye
mwenzake, ameitimiza sheria.
Warumi 13,8

Let each of you look not only to his own interests,
but also to the interests of others.
Philippians 2:4 (ESV)

Owe no one anything, except to love each other,
for the one who loves another has fulfilled the law.
Romans 13:8 (ESV)

Neno la Jumanne, 12. Agosti 2014

Ghafula sauti kama mvumo
mkubwa wa upepo uliotoka mbinguni,
ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi.
Zikatokea ndimi kama za moto
zilizogawanyika na kukaa juu ya kila mmoja wao.
Matendo ya Mitume 2,2-3

Wanafunzi wakajawa na furaha na Roho Mtakatifu.
Matendo ya Mitume 13,52

Suddenly there came from heaven
a sound like a mighty rushing wind,
and it filled the entire house where they were sitting.
And divided tongues as of fire appeared to them
and rested on each one of them.
Acts 2:2-3 (ESV)

The disciples were filled with joy and with the Holy Spirit.
Acts 13:52 (ESV)

Neno la Alhamisi, 14. Agosti 2014

Katika siku hiyo watauambia Yerusalemu,
"Usiogope, Ee Sayuni, Usiiache mikono yako ilegee.
BWANA Mungu wako yu pamoja nawe,
yeye ni mwenye nguvu kuokoa.
Atakufurahia kwa furaha kubwa,
atakutuliza kwa pendo lake, atakufurahia kwa kuimba."
Sefania 3,16-17

au kwa nchi,
kwa kuwa ndipo mahali pake pa kuwekea miguu,
au kwa Yerusalemu, kwa kuwa ndio mji wa Mfalme Mkuu.
Mathayo 5,35

Fear not, O Zion;
let not your hands grow weak.
The Lord your God is in your midst,
a mighty one who will save.
Zephaniah 3:16-17 (ESV)

Jerusalem is the city of the great King.
Matthew 5:35

Neno la Ijumaa, 1. Agosti 2014

Ndipo Yesu akawaambia, "Msiogope.
Nendeni mkawaambie ndugu zangu waende Galilaya,
ndiko watakakoniona."

Mathayo 28,10

Paulo akaandika:

Kristo akawatokea wale ndugu
waamini zaidi ya 500 kwa pamoja,
ambao wengi wao bado wako hai, ingawa wengine
wamelala.

1 Wakorinto 15,6

Jesus said to the women,
Do not be afraid;
go and tell my brothers to go to Galilee,
and there they will see me.

Matthew 28:10 (ESV)

Paul writes:

Christ appeared
to more than five hundred brothers at one time,
most of whom are still alive,
though some have fallen asleep.

1 Corinthians 15:6 (ESV)

Neno la Jumapili, 3. Agosti 2014

Usiseme,
"Nitamtenda kama alivyonitenda mimi,
nitamlipiza mtu yule kwa kile alichonitendea."

Mithali 24,29

Usishindwe na ubaya, bali uushindeni ubaya kwa wema.

Warumi 12,21

Do not say, "I will do to him as he has done to me;
I will pay the man back for what he has done."

Proverbs 24:29 (ESV)

Do not be overcome by evil,
but overcome evil with good.

Romans 12:21 (ESV)

Neno la Jumamosi, 30. Agosti 2014

BWANA anatukumbuka na atatubariki.

Zaburi 115,12

Kristo asema:

Kondoo Wangu huisikia sauti Yangu nami nawajua,
nao hunifuata, nami ninawapa uzima wa milele.

Yohana 10,27-28

The Lord has remembered us;
he will bless us.

Psalms 115:12

Christ says:

My sheep hear my voice,
and I know them,
and they follow me.
I give them eternal life.

John 10:27-28 (ESV)

Neno la Alhamisi, 28. Agosti 2014

"Kama vile mbingu mpya na nchi mpya ninazozifanya
zitakavyodumu mbele zangu," asema BWANA,
"ndivyo jina lenu na wazao wenu watakavyodumu."

Isaya 66,22

Paulo aandika kuhusu Israeli:

Ikiwa kukataliwa kwao ni kupatanishwa kwa ulimwengu,
kukubaliwa kwao si kutakuwa ni uhai baada ya kufa?

Warumi 11,15

As the new heavens and the new earth that I make
shall remain before me, says the Lord,
so shall your offspring and your name remain.

Isaiah 66:22 (ESV)

Paul writes about Israel:

If their rejection means the reconciliation of the world,
what will their acceptance mean but life from the dead?

Romans 11:15 (ESV)

Neno la Jumanne, 5. Agosti 2014

Kwa hiyo akainuka akala na kunywa.
Akiwa ametiwa nguvu na kile chakula,
akasafiri siku arobaini mchana
na usiku mpaka akafika Horebu,
mlima wa Mungu.
1 Wafalme 19,8

Yesu akasema:

Chakula changu ni kufanya mapenzi ya Mungu
ambaye amenituma na kuikamilisha kazi yake.
Yohana 4,34

Elijah arose and ate and drank,
and went in the strength of that food
forty days and forty nights
to Horeb, the mount of God.
1 Kings 19:8 (ESV)

Jesus said:

My food is to do the will of him who sent me
and to accomplish his work.
John 4:34 (ESV)

Neno la Alhamisi, 7. Agosti 2014

Yesu akawakaribisha umati wa watu
na kunena nao kuhusu Ufalme wa Mungu na kuwaponya
wale wote waliokuwa wanahitaji uponyaji.
Luka 9,11

Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu,
kwa sababu Mungu alimtuma
Mwanawe wa pekee ulimwenguni,
ili tupate uzima kwa Yeye.
1 Yohana 4,9

Jesus welcomed the crowds
and spoke to them of the kingdom of God
and cured those who had need of healing.
Luke 9:11 (ESV)

In this the love of God was made manifest among us,
that God sent his only Son into the world,
so that we might live through him.
1 John 4:9 (ESV)

Neno la Jumanne, 26. Agosti 2014

Haki yangu inakaribia inakuja mbio,
wokovu wangu unakuja, nao mkono
wangu utaleta hukumu kwa mataifa.
Isaya 51,5

Wote wametenda dhambi
na kupungukiwa na utukufu wa Mungu,
wanahesabiwa haki bure kwa
neema Yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu.
Warumi 3,23-24

My righteousness draws near,
my salvation has gone out,
and my arms will judge the peoples.
Isaiah 51:5 (ESV)

There is no distinction:
for all have sinned and fall short of the glory of God,
and are justified by his grace as a gift,
through the redemption that is in Christ Jesus.
Romans 3:22-24 (ESV)

Neno la Jumapili, 24. Agosti 2014

Kama ilivyoandikwa:
"Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa,
tumehesabiwa kama kondoo wa kuchinjwa."
Lakini katika mambo haya yote tunashinda,
naam na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda.
Warumi 8,36-37

Wale wanaoteswa sawasawa na mapenzi ya Mungu,
wajikabidhi kwa Mwumba wao
aliye mwaminifu huku wakizidi kutenda mema.
1 Petro 4,19

As it is written,
"For your sake we are being killed all the day long;
we are regarded as sheep to be slaughtered."
No, in all these things we are more than conquerors
through him who loved us.
Romans 8:36-37

Let those who suffer according to God's will
entrust their souls to a faithful Creator while doing good.
1 Peter 4:19 (ESV)

Neno la Jumamosi, 9. Agosti 2014

Lakini ni lazima urudi kwa Mungu wako,
dumisha upendo na haki,
nawe umngojee Mungu wako siku zote.

Hosea 12,6

Hii ndiyo amri Yake,
kwamba tuliamini Jina la Mwanawe, Yesu Kristo
na kupendana sisi kwa sisi kama Yeye alivyotuamuru.

1 Yohana 3,23

So you, by the help of your God, return,
hold fast to love and justice,
and wait continually for your God.

Hosea 12:6 (ESV)

This is his commandment,
that we believe in the name of his Son Jesus Christ
and love one another, just as he has commanded us.

1 John 3:23 (ESV)

Neno la Jumatatu, 11. Agosti 2014

Nimeandika kwa ajili yao mambo
mengi kuhusu sheria yangu,
lakini wameziangalia kama kitu cha kigeni.

Hosea 8,12

Ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza
Yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru,
bali fikira zao zimekuwa batili
na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza.

Warumi 1,21

Were I to write for Israel my laws by the ten thousands,
they would be regarded as a strange thing.

Hosea 8:12

Although they knew God,
they did not honor him as God or give thanks to him,
but they became futile in their thinking,
and their foolish hearts were darkened.

Romans 1:21 (ESV)

Neno la Ijumaa, 22. Agosti 2014

BWANA akaweka wimbo mpya kinywani mwangu,
wimbo wa sifa kwa Mungu wetu. Wengi wataona
na kuogopa na kuweka tumaini lao kwa BWANA.

Zaburi 40,3

Tarajio la mwenye haki ni furaha,
bali matumaini ya mwovu huwa si kitu.

Mithali 10,28

The Lord put a new song in my mouth,
a song of praise to our God.
Many will see and fear,
and put their trust in the Lord.

Psalms 40:3 (ESV)

The hope of the righteous brings joy,
but the expectation of the wicked will perish.

Proverbs 10:28 (ESV)

Neno la Jumatano, 20. Agosti 2014

Usimchukie ndugu yako moyoni mwako.
Karipia jirani yako kwa uwazi ili usishiriki hatia yake.

Mambo Ya Walawi 19,17

Angalieni sana mtu ye yote asiikose neema ya Mungu na
kwamba shina la uchungu lisije
likachipuka na kuwasumbua na
watu wengi wakatiwa unajisi kwa hilo.

Waebrania 12,15

You shall not hate your brother in your heart,
but you shall reason frankly with your neighbor,
lest you incur sin because of him.

Leviticus 19:17 (ESV)

See to it that no one fails to obtain the grace of God;
that no "root of bitterness" springs up and causes trouble,
and by it many become defiled.

Hebrews 12:15 (ESV)

Neno la Jumatano, 13. Agosti 2014

Mwili wake ukauawa, lakini akafanywa hai katika Roho.
1 Petro 3,18

Ikiwa Roho wa Mungu aliyemfufua
Yesu kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu,
Yeye aliyemfufua Kristo Yesu
kutoka kwa wafu ataihuisha pia miili yenu ambayo hufa,
kwa njia ya Roho Wake akaaye ndani yenu.
Warumi 8,11

Christ was put to death in the flesh
but made alive in the spirit.
1 Peter 3:18 (ESV)

If the Spirit of him
who raised Jesus from the dead dwells in you,
he who raised Christ Jesus from the dead
will also give life to your mortal bodies
through his Spirit who dwells in you.
Romans 8:11 (ESV)

Neno la Jumatatu, 18. Agosti 2014

Mataifa yanayowazunguka yaliyobakia watakapojua kuwa
Mimi BWANA nimejenga tena kile
kilichoharibiwa na nimepanda tena kile kilichokuwa ukiwa.
Ezekieli 36,36

Mwanzi uliopondeka hatauvunja
na utambi ufukao moshi hatauzima.
Kwa uaminifu ataleta haki.
Isaya 42,3

The nations that are left all around you
shall know that I am the Lord;
I have rebuilt the ruined places
and replanted that which was desolate.
Ezekiel 36:36 (ESV)

A bruised reed he will not break,
and a faintly burning wick he will not quench;
he will faithfully bring forth justice.
Isaiah 42:3 (ESV)

Neno la Ijumaa, 15. Agosti 2014

Yesu akawaambia wanafunzi wake:
Nikienda na kuwaandalia makao,
nitarudi tena na kuwachukua mkae pamoja nami,
ili mahali nilipo, nanyi mpate kuwepo.
Yohana 14,3

Kisha mhalifu akasema, "Bwana Yesu,
unikumbuke utakapokuja katika Ufalme Wako."
Yesu akamjibu, "Amin, nakuambia,
leo hii utakuwa pamoja nami Paradiso"
Luka 23,42-43

Jesus said to the disciples:

If I go and prepare a place for you,
I will come again and will take you to myself,
that where I am you may be also.
John 14:3 (ESV)

The criminal said,
Jesus, remember me when you come into your kingdom.
And he said to him,
Truly, I say to you, today you will be with me in Paradise.
Luke 23:42-43 (ESV)

Neno la Jumamosi, 16. Agosti 2014

Ndipo nitatakasa midomo ya mataifa, kwamba wote
waweze kuliitia
jina la BWANA na kumtumikia kwa pamoja.
Sefania 3,9

Yohana akaandika:
Kisha nikamwona malaika mwingine akiruka juu angani,
naye alikuwa na Injili ya milele
ya kuwatangazia wale waishio duniani,
yaani, kwa kila taifa, kabila, lugha na jamaa.
Ufunuo wa Yohana 14,6

At that time I will change
the speech of the peoples to a pure speech,
that all of them may call upon the name of the Lord
and serve him with one accord.
Zephaniah 3:9

John writes:

I saw another angel flying directly overhead,
with an eternal gospel
to proclaim to those who dwell on earth,
to every nation and tribe and language and people.
Revelation 14:6 (ESV)